HABARI na MATUKIO

Toleo Na. 4 | Tanzania Fertilizer Regulatory Authority | tfra_official | tfra_official | Juni 2022

JARIDA LA KILA MWEZI LA MAMLAKA YA UDHIBITI WA MBOLEA TANZANIA

Matunda mikataba ya wawekezaji iliyosainiwa na Rais Samia Dubai yawa dhahiri

Balozi James Bwana (wanne kutoka kulia) akiwa katika picha ya pamoja na viongozi wa serikali na viongozi wa kampuni ya Rokosan na wabia wake mara baada ya kufungua warsha iliyolenga kuitambulisha kampuni hiyo iliyofanyika tarehe 25 Mei, 2022 katika ukumbi wa Four Points by Sheraton Jijini Dar Es Salaam. Wa kwanza kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) Dkt. Stephan Ngailo.

NDANI>>

Itracom fertilizer Limited suluhisho changamoto ya mbolea nchini 5

RUZUKU YA MBOLEA KUTOLEWA MSIMU UJAO WA KILIMO 2022/2023 7

Mwekezaji kutoka Slovakia kujenga kiwanda cha mbolea Pwani 9

Matunda mikataba ya wawekezaji iliyosainiwa na Rais Samia Dubai yawa dhahiri

Imeelezwa kwamba ujio wa mwekezaji wa kampuni ya Rokosan ya nchini Slovakia ni matokeo ya moja kati ya mikataba iliyosainiwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassani alipofanya ziara ya kikazi nchini Dubai wakati wa maonesho ya Dubai -Expo 2020.

Hayo yamebainishwa na Balozi James Bwana aliyemwakilisha Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Balozi Joseph Sokoine kwenye ufunguzi wa warsha iliyoandaliwa na kampuni hiyo kwa lengo la kuitambulisha kampuni na bidhaa itakayokuwa ikizalisha iliyofanyika tarehe 25 Mei, 2022 katika ukumbi wa New Africa Hote Jijini Dar Es Salaam.

Balozi James Bwana alieleza kuwa mazingira rafiki yaliyowekwa na Rais Samia yameendelea kuwavutia wawekezaji wengi wanaoendelea kuonesha nia na kuja kuwekeza nchini, kampuni ya Rokosan ikiwa ni miongoni mwao.

Balozi James Bwana (wanne kutoka kulia) akiwa katika picha ya pamoja na viongozi wa serikali na viongozi wa kampuni ya Rokosan na wabia wake iliyolenga kuitambulisha kampuni hiyo iliyofanyika tarehe 25 Mei, 2022 katika ukumbi wa Four Points by Sheraton Jijini Dar Es Salaam. Wa kwanza kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) Dkt. Stephan Ngailo.

Balozi James Alisema uwepo wa kiwanda cha mbolea kinachotarajiwa kujengwa wilayani Pwani kutaimarisha hali ya kimazingira ya nchi kutokana kiwanda hicho kutumia malighafi za asili zinazopatikana katika mazingira ya kawaida ambapo awali zilikuwa zikitupwa kama uchafu.

Alisema, kutokana na matumizi hayo ya taka hizo zilizokuwa zikisababisha uchafunzi wa mazingira sasa zitatumika kama malighafi na hivyo kuimarisha uchumi wa wananchi mara baada ya kuuza taka hizo kiwandani lakini pia zitapunguza uchafuzi wa mazingira.

Aliendelea kusema, uwepo wa kiwanda hicho nchini utaongeza usalama wa chakula na kupunguza madhara yaliyotokana na matumizi mabaya ya mbolea zenye kemikali ambazo zimeharibu afya ya udongo kwa kiasi kikubwa.

Aidha, Balozi James alisema, kutokana na aina ya mbolea itakayozalishwa kiwandani hapo kutokuwa na madhara kwa udongo na mazao, mazao yatakayopatikana kufuatia matumizi ya mbolea hiyo yatapata soko la uhakika nje ya nchi na hivyo kuliingizia taifa fedha za kigeni na kuongeza mchango wa Sekta ya kilimo kwenye pato la Taifa.

Balozi James Bwana (wanne kutoka kulia) akiwa katika picha ya pamoja na viongozi wa serikali na viongozi wa kampuni ya Rokosan na wabia wake iliyolenga kuitambulisha kampuni hiyo iliyofanyika tarehe 25 Mei, 2022 katika ukumbi wa Four Points by Sheraton Jijini Dar Es Salaam. Wa kwanza kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) Dkt. Stephan Ngailo.

Matunda mikataba ya wawekezaji iliyosainiwa na Rais Samia Dubai yawa dhahiri

Washiriki wakifuatilia mada wakati wa warsha ya kuitambulisha kampuni hiyo iliyofanyika tarehe 25 Mei, 2022 katika ukumbi wa Four Points by Sheraton Jijini Dar Es Salaam. Wa kwanza kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) Dkt. Stephan Ngailo.

Washiriki wakifuatilia mada wakati wa warsha ya kuitambulisha kampuni hiyo iliyofanyika tarehe 25 Mei, 2022 katika ukumbi wa Four Points by Sheraton Jijini Dar Es Salaam.

Balozi James Bwana alihitimisha hotuba yake kwa kuwaalika wawekezaji wengine kufika nchini na kuwekeza katika sekta mbalimbali zikiwemo sekta ya kilimo, sekta ya Utalii, sekta ya Madini na kwingineko kadri watakavyoona inafaa.

Akizungumza katika warsha hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) Dkt. Stephan Ngailo alisema, moja kati ya majukumu ya Mamlaka ni kuhamasisha uwekezaji wa ndani wa viwanda vya mbolea ili kuwapunguzia wakulima changamoto ya upatikanaji wa mbolea.

Washiriki wakifuatilia mada wakati wa warsha ya kuitambulisha kampuni ya Rokosan itakayojenga kiwanda cha mbolea ya asili mkoani Pwani iliyofanyika tarehe 25 Mei, 2022 katika ukumbi wa Four Points by Sheraton Jijini Dar Es Salaam.

Dkt. Ngailo alisema, kufuatia changamoto mbalimbali zikiwemo za ugonjwa wa uvico-19 na vita kati ya Ukraini na Urusi ambayo ni miongoni mwa mataifa yanayozalisha mbolea kwa wingi kumepelekea kuwepo kwa changamoto ya bei na upatikanaji wa mbolea kutokana na ukweli kwamba asilimia 90 ya mbolea inayotumika nchini kuingizwa kutoka nje ya nchi.

Dkt. Ngailo aliwahakikishia ushirikiano wa kutosha wawekezaji hao na kuhakikisha mchakato mzima wa kuanzisha kiwanda hicho cha mbolea ya asili (organic fertilizer) unakamilika na mradi unaanza kwa wakati.

Akizungumzia suala la kiwango cha mbolea kinachohitajika nchini kwa mwaka, Dkt. Ngailo alisema tani laki saba (700000) zinatumika kwa mwaka na kubainisha kuwa kiasi hicho cha matumizi ni kidogo kutokana na wakulima wengi kutokuwa na uwezo wa kununua mbolea

Matunda mikataba ya wawekezaji iliyosainiwa na Rais Samia Dubai yawa dhahiri

kutokana na bei yake kuwa juu.

Aidha, Dkt Ngailo aliwataka wadau pamoja na wawekezaji kuendelea kuhamasisha matumizi ya mbolea kwa wakulima kwani baadhi yao hawatumii mbolea kutokana na kutokuwa na uelewa wa tija inayotokana na matumizi ya mbolea kwenye kilimo pamoja na wengine kuwa na Imani mgando juu ya matumizi hayo ya mbolea na kueleza matumizi sahihi ya mbolea hayana madhara kwa mlaji.

Akizungumzia suala la ubora wa mbolea itakayozalishwa na kiwanda hicho, Dkt. Ngailo aliwahakikisha watanzania na wakulima kwa ujumla kuwa mbolea itakayozalishwa na kiwanda hicho itapimwa ili kujiridhisha na viwango vya ubora vitakavyopatikana kwenye mbolea hiyo kabla ya kuanza kutuka na wakulima kwenye shughuli zao za kilimo.

Kwa upande wa soko, Dkt Ngailo alisema kiwanda hicho kinatarajia kuzalisha kiasi cha lita milioni ishirini (lita 20000000) kwa mwaka na kubainisha kuwa kiwanda kingine cha Itracom kinachojengwa Jijini Dodoma na kuzalisha tani laki sita za mbolea kwa mwaka soko lake ni la uhakika.

Amesema uhakika wa soko unatokana na malighafi zitakazotumika katika uzalishaji wa mbolea kupatikana nchini kwa wingi na hivyo kuwa na uhakika kuwa bei zitakazouzia bidhaa hizo zitakuwa ni zile ambazo wakulima wanazimudu ikiwa ni pamoja na kuziuzia nchi jirani kiasi cha mbolea kinachobaki

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) Dkt. Stephan Ngailo akizungumza jambo mbele ya washiriki wa warsha iliyolenga kuitambulisha kampuni ya Rokosan na wabia wake iliyofanyika tarehe 25 Mei, 2022 katika ukumbi wa Four Points by Sheraton Jijini Dar Es Salaam

baada ya kutosheleza mahitaji ya ndani.

Akizungumzia uzoefu wa kampuni hiyo kwenye biashara ya mbolea Mkurugenzi wa Kampuni ya Rokosan, Adam Zo'ke alisema kampuni yake ina miaka 20 kwenye biashara hiyo na kwamba inatambulika kwenye umoja wa Ulaya na Afrika na kukiri anatarajia kufanya Zaidi biashara ya mbolea barani Afrika.

Alisema mbolea inayozalishwa kiwandani hapo itatokana na vitu vya asili kama vile manyoya ya kuku, kwato, pembe za ng'ombe na wanyama wengine, samadi ya mifugo na nyinginezo jambo litakalosaidia katika kutunza mazingira kwa kiasi kikubwa.

Alisema mbolea hiyo ni rafiki kwa udongo na walaji kutokana na utengenezaji wake kutohusisha kemikali na kwamba ikitumika kwa muda mfupi hurejesha afya ya udongo iliyopotea kutokana na sababu mbalimbali.

Matokeo ya kutumia mbolea itakayozalishwa kiwandani hapo ni pamoja na kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao hivyo kuwa na uhakika wa chakula, kufungua soko kwa wafugaji kuuza malighafi kwa ajili ya kiwanda hicho, kuboresha bioanuai katika udongo, na ufufuaji wa ardhi ya kilimo iliyoathirika kwa matumizi ya muda mrefu.

Pamoja na hayo Dr. Adam alieleza manufaa mengine kuwa ni kuongeza fursa za ajira ambapo alibainisha kuwa pindi ujenzi utakapoanza watanzania 150 wataajiriwa ili kufanya kazi za ujenzi kiwandani hapo na baada ya ujenzi kukamilika wanatarajia kutoa ajira za kudumu 1000 kwa watanzania na ajira 12 kwa wataalamu kutoka nje ya nchi.

Itracom fertilizer Limited suluhisho changamoto ya mbolea nchini

Imeelezwa kuwa kujengwa kwa kiwanda kikubwa cha mbolea cha Itracom Fertilizer Ltd nchini kutatatua changamoto ya upatikanaji na bei ya mbolea kwa wakulima nchini.

Kutokana na uzalishaji wa ndani wa mbolea kuwa mdogo ambapo asilimia kumi pekee ndiyo inayozalishwa na viwanda vya ndani na asilimia 90 (90%) kuingizwa kutoka nje ya nchi na uwepo wa changamoto ya ugonjwa wa Uvico -19 na vita baina ya Urusi na Ukrein kumesababisha bei za mbolea kupanda kupita kawaida na hivyo kupelekea wakulima kushindwa kuhimili gharama ya mbolea.

Hayo yalibainishwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Dkt. Stephan Ngailo aliposhiriki maadhimisho ya siku ya mkulima yaliyofanyika katika shamba la mfano la mpunga lililolenga kuonesha faida ya matumizi ya mbolea inayozalishwa na kiwanda hicho.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Utafiti Tanzania Dkt. Godfrey Mkamilo (wa kwanza kulia) akieleza matokeo ya jaribio la mbolea aina ya fomi pandia na fomi kuzia baada ya kuitumia katia mashamba darasa kwa Mkuu wa Wilaya ya Kilosa Majid Hemed Mwanga (wa kwanza kushoto) tarehe 19/5/2022 alipotembea ili kujionea matokeo ya mbolea itakayozalishwa na kiwanda cha mbolea cha Intracom

Dkt. Ngailo alisema ujenzi wa kiwanda cha Itracom Fertilizer ni matokeo ya Diplomasia ya Uchumi ya Rais Samia Suluhu Hassan iliyowavutia wawekezaji kutoka nchini Burundi kuja kuweka nchini.

Aliendelea kusema, kiwanda

Mkurugenzi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) Dkt. Stephan Ngailo akizungumza jambo wakati wa hafla ya jaribio la mbolea itakayozalishwa na kiwanda cha Intracom kinachojengwa Jijini Dodoma kikiwa na uwezo wa kuanza kuzalisha tani laki sita za mbolea kwa mwaka

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Taanzania (TFRA) akizungumza jambo mbele ya Mkuu wa Wilaya ya Kilosa Majid Hemed Mwanga (haonekani pichani) walipokuwa wakikagua mashamba kujionea tofauti ya uzalishaji katika mashamba yaliyopandwa na kukuziwa kwa mbolea aina ya DAP na UREA na mbolea inayozalishwa na kiwanda cha Intracom kinachozalisha mbolea yenye mchanganyiko wa samadi na kemikali(organic fertilizer) tarehe 19/5/2022

cha itracom kitazalisha tani laki sita (600,000) za mbolea na kubainisha mahitaji ya mbolea kwa mwaka ni takribani

Aidha, Dkt. Ngailo amewataka wawekezaji wengine kutosita kufika nchini ili kuwekeza kwani Tanzania imejaliwa kuwa utashi wa kisiasa pamoja na uwepo wa malighafi za kutosha kwa ajili ya uzalishaji wa mbolea ikiwa ni pamoja na uwepo wa nishati ya uhakika, uwepo wa nguvu kazi pamoja na uhakika wa soko ambao ni wakulima wanaotumia bidhaa hiyo.

Kwa upande wa Mkurugenzi wa kiwanda cha Itracom Fertilizer Limited, Nduwimana Nazaire aliwahakikishia wakulima wa Ilonga upatikanaji wa mbolea pamoja na bei nzuri ukilinganisha na aina nyingine za mbolea zinazopatikana nchini.

“Msiwe na shida na mashaka mbolea itapatikana na ikitosheleza mahitaji ya

Itracom fertilizer Limited suluhisho changamoto ya mbolea nchini

Viongozi mbalimbali walioshiriki hafla ya jaribio la mbolea itakayozalishwa na kiwanda cHa Intracom wakifuatilia hafla hiyo iliyofanyika katika ofisi za kijiji cha Ilonga tarehe 19 Mei, 2022 wilayani Kilosa.

ndani ndipo tutaisafirisha kwenda nje ya nchi” Nazaire anasema.

Amesema kiwanda anachokisimamia kinazalisha mbolea yenye mchanganyiko wa samadi na kemikali kwa uwiano wa 50/50 ambayo haina madhara kwa udongo naikitumika kwa miaka miwili au mitatu udongo utazalisha kama kawaida hata usipotumia mbolea.

Ameendelea kusema, kwao ni furaha kutoa huduma ya mbolea kwa watanzania na kueleza, mkulima akichoka sana wakati wa kuandaa na kulima mashamba atausahau uchovu huo wakati wa kuvuna kutokana na matokeo mazuri atakayoyapata kufuatia matumizi ya mbolea iitakayozalishwa kiwandani hapo.

Nazaire alisema kiwanda hicho kinatarajia kuanza uzalishaji ifikapo Mwezi wa saba ambapo wataanza kuzalisha tani laki sita za mbolea zitakazoendelea kuongezeka mpaka kufikia uzalishaji wa tani milioni moja na nusu (tani 1500000).

Mkurugenzi wa kiwanda cha Intracom Fertilizer Limited, Nduwimana Nazaire akizungumza jambo wakati wa hafla ya Majaribio ya mbolea itakayozalishwa na kiwanda chake kinachotarajiwa kuanza uzalishaji mwezi Julai 2022 na kuzalisha kiasi cha tani laki sita za mbolea kwa mwaka

RUZUKU YA MBOLEA KUTOLEWA MSIMU UJAO WA KILIMO 2022/2023

- Wafanyabiashara kusajiliwa na TFRA kwenye mfumo maalum wa ruzuku

Waziri wa Kilimo Hussein Bashe akiwasilisha makadirio na matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 Bungeni Jijini Dodoma tarehe 17 May, 2022.

Imeelezwa kuwa serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 150 kwa ajili ya kutoa ruzuku ya mbolea kwa wakulima wa mazao yote nchini kwa msimu wa kilimo wa Mwaka 2022/ 2023.

Hayo yamebainishwa leo tarehe 17 Mei, 2022 na Waziri wa kilimo Husen Bashe alipokuwa akiwasilisha hotuba ya bajeti ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2022/2023 katika kikao cha bunge cha 13 kinachoendelea jijini Dodoma.

Waziri wa Kilimo Hussein Bashe akiwasilisha makadirio na matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 Bungeni Jijini Dodoma tarehe 17 May, 2022.

Waziri Bashe ameziagiza kampuni na viwanda vyote vya mbolea nchini kusajiliwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) ifikapo tarehe 31 Mei, 2022 ili kurahisisha utoaji na usimamizi wa ruzuku.

Akielezea namna ya utoaji wa ruzuku hizo Waziri Bashe alisema mifuko ya mbolea itawekwa barcode nalabel ya ruzuku ili kutofautisha na mbolea zitakazoendelea kuuzwa sokoni bila ruzuku.

Pamoja na hayo, Waziri

RUZUKU YA MBOLEA KUTOLEWA MSIMU UJAO WA KILIMO 2022/2023

Bashe amesema kampuni yeyote ambayo haitatekeleza agizo hilo na kukubali kutumia mfumo utakaowekwa na TFRA wa kusimamia na kusajili kampuni na mawakala kwa kuweka eneo la biashara kwenye maduka na ghala zao mikoani serikalihaitosita kuwafutia leseni zao za biashara.

Aidha, Waziri Bashe amebainisha kuwa mfumo huo wa mbolea ya ruzuku utawapa kipaumbele wazalishaji wa ndani ili kulinda viwanda vya ndani, ajira na usalama wa chakula.

Amesema, Wizara itaendelea kuwalinda na kuwawezesha wawekezaji wa viwanda vya ndani ikiwepo intracom fertilizer Limited chenye uwezo wa kuzaisha tani 600,000 (laki sita) mbolea pamoja na kushirikiana na kuwezesha upatikanaji wa vivutio vya uwekezaji kwa kiwanda cha mbolea Minjingu ili kuongeza uwezo wake wa kuzalisha kutoka tani 100,000 za sasa.

Vilevile Waziri Bashe amewahakikishia wazalishaji wadogo wa mbolea hai organic na chokaa kuwa itaendelea kuwalea, kuwalinda, na kuwahakikishia masoko ili kupunguza gharama za kuagiza aina hiyo ya mbolea kutoka nje ya nchi na kuwataka wazalishaji wadogo wa aina hiyo ya mbolea kufika wizarani ili kuweza kusaidiwa.

Akizungumzia manufaa ya ziara za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuimarisha mahusiano na nchi za Afrika Mashariki, waziri Bashe amesema ni pamoja na kumpata mwekezaji mkubwa wa kiwanda cha mbolea cha Intracom Fertilizer Limited kinachojengwa Jijini Dodoma na mwekezaji kutoka nchini Burundi.

Amesema uwekezaji wa ujenzi wa kiwanda hicho unagharimu kiasi cha dola za Marekani milioni 180 huku kikitarajiwa kuzalisha kiasi cha tani laki sita (600000) za mbolea kwa mwaka na kutoa ajira za kudumu kwa watanzania 3000.

Ameendelea kusema, wizara imeendelea kuratibu uzalishaji na uingizaji wa mbolea nchini ambapo tani 436,452 za mbolea zimepatikana kwa msimu wa kilimo wa 2021/2022 ikiwa ni asilimia 63 (63%) ya mahitaji yote ya mbolea na kubainisha kuwa tani 274000 zimeingizwa kutoka nje ya nchi na tani 43000 zimezalishwa katika viwanda vya ndani wakati kiasi cha tani 117 900 ni bakaa ya msimu uliopita wa kilimo.

Naibu Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde akichangia mada wakati wa kikao cha 12 cha Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Jijini Dodoma.

Mwekezaji kutoka Slovakia kujenga kiwanda cha mbolea Pwani

Mkurugenzi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) Dkt. Stephan Ngailo akizungumza jambo mbele ya wajumbe walioshiriki kikao baina ya TFRA na wawekezaji kutoka nchini Slovakia tarehe 24 Mei, 2022

Mwekezaji kutoka nchini Slovakia kupitia kampuni la ROKOSAN ameonesha nia ya kujenga kiwanda cha mbolea katika eneo la Soga Wilaya ya Kibaha mkoani Pwani.

Mwekezaji huyo Dkt. Adam Seo'ke ambaye aliambatana na wadau wengine kutoka makampuni mawili ya hapa nchini KOM na Selphina ameonesha nia yake wakati alipotembelea ofisi za Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) jijini Dar es Salaam leo tarehe 24 Mei, 2022 na kufanya mazungumzo na Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka Dkt. Stephan Ngailo

Akizungumza wakati wa kikao hicho Dkt Ngailo amesema matumizi ya mbolea kwa Tanzania yamepungua kutokana na bei ya bidhaa hiyo kuwa juu kiasi ambacho wakulima wadogo wanashindwa kumudu gharama ya bidhaa hiyo.

"Ujenzi wa kiwanda cha mbolea mkoani Pwani ni habari njema kwa wakulima wa Tanzania kwani utaongeza uzalishaji wa ndani na hivyo kumpunguzia mkulima makali ya kununua bidhaa hiyo kwa bei kubwa ambayo wengi wao hawawezi kumudu" Alisema Dkt.Ngailo.

Amesema maono ya serikali ni kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha mbolea Afrika Mashariki na Kati na kuwahakikishia wawekezaji hao kuwa soko la bidhaa hiyo nchini ni la uhakika na kueleza pindi itakapotosheleza kwa matumizi ya ndani ya nchi itauzwa nchi jirani kama vile Demokrasia ya watu wa Kongo (DRC), Burundi, Uganda, Rwanda na nchi nyinginezo.

Pamoja na hayo, Dkt. Ngailo aliwahakikishia wawekezaji hao ushirikiano wa kutosha katika kuhakikisha hazma

Wajumbe wa kikao baina ya TFRA na wawekezaji wa kutoka Slovakia wakimsikiliza Mkurugenzi wa Uzalishaji wa Ndani na Ununuzi wa Mbolea kwa Pamoja Josephy Charos akizungumza jambo wakati wa kikao kilichofanyika katika ukumbi wa Mkutano wa TFRA Jijini Dar es Salaam tarehe 24 Mei, 2022 .

Mwekezaji kutoka Slovakia kujenga kiwanda cha mbolea Pwani

yao ya kuwekeza kwenye kiwanda cha mbolea inatimia.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa uzalishaji wa ndani na ununuzi wa mbolea kwa pamoja Joseph Charos aliwashauri wawekezaji kuwekeza katika kuitangaza bidhaa watakayozalisha kwa vitendo kwani upatikanaji wa wateja utatokana na namna walivyoielewa bidhaa husika.

Akizungumza kwa niaba ya wajumbe walioshiriki kikao hicho kutoka kwa wawekezaji hao Dr. Adam Seo'ke amesema kiwanda wanachotarajia kukijenga kitakuwa kikizalisha mbolea ya asili ya kimiminika (organic folier fertilizer) na kuuzwa kwa bei nafuu kwani itazalishwa kwa kutumia malighafi za asili.

Mkurugenzi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) Dkt. Stephan Ngailo (wa pili kutoka kulia mbele) akiwa katika picha ya pamoja na wawekezaji waliofika kueleza nia ya kutaka kujenga kiwanda cha mbolea Mkoani Pwani.

Amesema, ujenzi wa kiwanda hicho utafungua fursa za ajira pamoja na kuwahakikishia watanzania uhakika wa chakula kutokana na mbolea hiyo kuongeza virutubisho vya kutosha kwenye udongo pasipo kuwa na athari zozote kwenye afya za walaji.

Wawekezaji wakifuatilia maelezo ya Mkurugenzi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) Dkt. Stephan Ngailo (hayupo pichani) kushoto ni Dkt. Adam Seo'ke, akifuatiwa na Stefan Seo'ke.

Aidha, Adam ameomba ushirikiano baina yao serikali na taasisi zinazosimamia tasnia ya mbolea ambapo alihakikishiwa kupata ushirikiano wa kutosha kutoka TFRA pamoja na taasisi nyingine serikalini.

Ujio wa wawekezaji wa kiwanda cha mbolea ni moja kati ya mikakati ya TFRA katika kuhakikisha uzalishaji wa ndani unaongezeka na hivyo kupunguza changamoto ya bei na upatikanaji wa mbolea nchini.

Mfanyabiashara wa mbolea kutoka Iran aonesha nia kuwekeza nchini

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Stephan Ngailo amekutana na balozi wa Tanzania nchini Kenya Dkt. John Stephen Simbachawene aliyemtembelea ofisini kwake leo tarehe 24 Mei, 2022.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Stephan Ngailo (kushoto), akifuatiwa na balozi wa Tanzania nchini Kenya Dkt. John Stephen Simbachawene na Mfanyabiashara wa Mbolea Mohammad Salimian walipokutana ofisini kwa Mkurugenzi wa mamlaka jijini Dar Es Salaam leo tar 24 Mei, 2022 .

Balozi Simbachawene amefika ofisini hapo akiambatana na mfanyabiashara wa mbolea kutoka nchini Irani anayejishughuulisha na biashaa ya mbolea aina ya Urea nchini Kenya Mohammad Salimian.

Akizungumza katika kikao hicho, Dkt. Ngailo alimkaribisha mwekezaji huyo na kueleza fuursa ya kufanya biashara hiyo nchini ipo na kumtaka kukamilisha taratibu zote zitakazomfanya aweze kujihusisha na biashara ya mbolea.

Akielezea taratibu hizo, Dkt. Ngailo alisema ni pamoja na kuwa na namba ya mlipa kodi (Tin number), cheti cha Usajili wa kampuni kutoka Brella, Mfanyabiashara

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Stephan Ngailo (mbele) akiwa katika kikao na balozi wa Tanzania nchini Kenya Dkt. John Stephen Simbachawene na mfanyabiashara wa mbolea Mohammad Salimian leo tarehe 24 Mei, 2022 Ofisini kwake Jijini Dar es Salaam.

Mfanyabiashara wa mbolea kutoka Iran aonesha nia kuwekeza nchini

mwenye ujuzi katika masuala ya kilimo na mbolea pamoja na kusajiliwa kwenye mfumo wa kielekroniki wa mbolea (FIS)

Aidha, Dkt. Ngailo alimshukuru Balozi Dkt. Simbachawene kwa juhudi kubwa za kutatua changamoto za upatikanaji na bei za mbolea zinazolikabili taifa na kumhakikishia ushirikiano wa kutosha katika kuhakikisha mfanyabiashara anafikia malengo yake.

Kwa upande wake, Balozi Simbachawene alieleza nia yake ya kufika ili kumtambulisha mfanya biashara Salimian aliyeonesha nia ya kufanya biashara ya mbolea nchini Tanzania.

Kwa upande wake mfanyabiashara Salimian alieleza kuwa uzalishaji wa mbolea aina ya Urea nchini Iran ni mkubwa hivyo anatarajia kuja nchini ili aweze kufanya biashara hiyo na kueleza kuwa nchi yao inawapa ahaueni wafanyabiashara ili waweze kununua bidhaa na kuuza nchi za nje.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Stephan Ngailo (wa tatu kutoka kushoto) kulia kwake ni balozi wa Tanzania nchini Kenya Dkt. John Stephen Simbachawene na kushoto kwake ni Mfanyabiashara wa mbolea Mohammad Salimian na wakurugenzi walioshiriki kikao cha utambulisho kilichofanyika Ofisini kwa Mkurugenzi jijini Dar es Salaam wakiwa katika picha mara baada ya kikao kwisha.

Ujenzi maabara ya mbolea wamkosha Katibu Mkuu Kilimo

Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Bw. Andrew Massawe amefurahishwa na ubora na hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa ujenzi wa mradi wa maabara ya kimataifa ya mbolea unaosimamiwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA).

Katibu Mkuu Masawe alitoa pongezi hizo hivi karibuni alipotembelea ofisi za mamlaka hiyo kwa lengo la kufuatilia maendeleo ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa maabara hiyo pamoja na kufuatilia utekelezaji wa maelekezo aliyotoa mwezi Novemba 30, 2022 kuhusu ujenzi wa maabara hiyo unaoendelea katika eneo la Kilimo III - Temeke Dar es salaam.

Pamoja na hayo aliitaka Menejimenti kuangalia uwezekano wa kuongeza idadi ya ghorofa ili kuweza kumudu kuwahudumia wateja wengi wenye mahitaji tofautitofauti yanayohusiana na kilimo kwa kuwa na taasisi mbalimbali ndani ya jingo moja.

Akizungumzia maendeleo ya ujenzi wa maabara hiyo, Charos alieleza kuwa, ujenzi wa umefikia asilimia 60 ambapo plasta kwenye kuta kwa ajili ya sakafu ya chini (ground floor) ikiwa ni pamoja na uwekeji wa miundombinu ya awali ya umeme na maji (First fix services) umekamilika na kuongeza kuwa umwagaji wa zege (slab) la sakafu ya pili pia umekamilika.

Kufuatia maelekezo yaliyoyatolewa na Katibu Mkuu Massawe ya kulifanya jengo hilo

Ujenzi maabara ya mbolea wamkosha Katibu Mkuu Kilimo

kuwa kitovu cha taarifa , huduma na habari zote zinazohusiana na mbolea nchini (fertilizer one stop centre), Mamlaka ilieleza kupokea maelekezo hayo na kuanza kuyafanyia kazi na hivyo kuifanya maabara kuwa ya kisasa na ya kuvutia na kuwa ni kituo cha ubora kuhusu masuala yote yanayohusu mbolea (fertilizer centre of excellence).

Pamoja na hayo Mwenyekiti wa Kamati ya Ujenzi Charos, alieleza kuwa Menejimenti imeendelea kushirikiana na Mshauri Elekezi kuona namna inavyoweza kuboresha muonekeno wa jengo (State of Art) hususan katika ghorofa mbili (2) zinazotarajiwa kuendelea kujengwa.

Aidha, kuhusu (fertilizer one stop centre) Mamlaka itashirikiana na Taasisi zingine zinazojihusha na shughuli za mbolea kwa ajili ya kufanya eneo hilo kuwa kitovu cha kutolea huduma zinazohusiana na mbolea na pembejeo kwa kuzingatia matumizi bora ya eneo lililobaki.

Akizungumzia gharama zilizotumika katika utekelezaji wa mradi huo, Charos alisema kufikia Machi 30, 2022 jumla ya Shilingi 746,016,267.43 kimetumika kwa ajili ya manunuzi ya vifaa na huduma mbalimbali kwenye eneo la ujenzi.

Ujenzi wa maabara ya kisasa ya mbolea nchini ni suala muhimu katika kwa mamlka kwa itaondoa changamoto ya muda katika upatikanaji wa taarifa za vipimo vya mbolea na kupunguza baadhi ya changamoto mbalimbali zinazoikabili Mamlaka katika kutekeleza majukumu yake.

KANDA YA KATI

TFRA KANDA YA KATI YATOA MFUNZO KWA WAFANYABIASHARA WA MBOLEA

Afisa Udhibiti Ubora, Steven Goss akitoa mada kwa wafanyabiashara 83 wa mbolea walioshiriki mafunzo ya matimizi sahihi ya mbolea yaliyofanyika katika ukumbi wa Tabora Manispaa tarehe 23 Mei, 2022 ili kuwajengea uwezo juu ya Sheria, kanuni na taratibu zinazosimamia tasnia ya mbolea nchini.

Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea nchini Kanda ya Kati ambayo imeanza kutekeleza majukumu yake kuanzi tarehe 01 Machi, 2022 imefanya mafunzo kwa Wafanyabiashara wa Mbolea (wamiliki na wauzaji) wapatao 201 katika vituo 4 tofauti kwa mwezi Mei, 2022.

Mafunzo hayo yalifanyika kwa siku tofautitofauti kama inavyooneshwa hapo chini;

- Tarehe 23/24 Mei 2022 kituo cha Tabora Manispaa (Uyui na Tabora DC - Wafanyabiashara 83
- Tarehe 25/26 Mei, 2022 Kituo cha Nzega (Nzega TC na Nzega DC) Wafanyabiashara 19
- Tarehe 26/27 Mei, 2022 Igunga DC jumla ya Wafanyabiashara 66 walishiriki na
- Tarehe 28/29 Mei, 2022 Urambo Jumla ya Wafanyabiashara 33 walishiriki.

Mafunzo yalijikita Sheria ya mbolea na kanuni zake ili kuwawezesha kufanya biashara kwa mujibu wa Sheria, Usajili wa mbolea, Maombi ya leseni kupitia mfumo wa FIS (Fertilizer Information System).

Mada nyingine ni matumizi sahihi ya mbolea na virutubishi vyake pamoja na Maandalizi ya utoaji mpya wa ruzuku ya mbolea kwa msimu wa kilimo wa 2022/2023 ambapo wafanyabiashara watakaoridhia kushiriki katika kufanya biashara ya mbolea ya ruzuku watapaswa kusajiliwa kwenye mfumo wa ruzuku unaosimamiwa na TFRA.

Kufuatia maelekezo ya Bodi ya Wakurugenzi walivyoelekeza katika kikao cha Mwezi April 2022 kuitaka Mamlaka kuboresha vyeti vya wanufaika wa mafunzo kwa kuweka picha zao kwenye vyeti

KANDA YA KATI

TFRA KANDA YA KATI YATOA MFUNZO KWA WAFANYABIASHARA WA MBOLEA

Wahitimu wa mafunzo kutoka Igunga DC wakiwa wametunukiwa vyeti vyao vya mafunzo ya mbolea

Akizungumza kwa niaba ya watumishi wa TFRA kanda ya kati Kaimu Meneja wa Kanda Joshua Ng'ondya alisema, wana Imani kupitia mafunzo hayo uzingatiaji wa Sheria na Kanuni za Mbolea utaongezeka hivyo wakulima kupata pembejeo zenye ubora hatimaye kuongeza tija ya uzalishaji na kipato.

Alisema, Kanda ya Kati itaendelea kushirikiana kwa ukaribu na Ofisi za Mikoa, Wilaya na Halmashauri ili kuhakikisha tasnia ya mbolea inasimamiwa kikamilifu.

Kwa upande wake, Mwakilishi kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Said Babu akifungua mafunzo kwa wafanyabiashara wa mbolea katika ukumbi wa Manspaa ya Tabora tarehe 23 mei 2022 alisisitiza umuhumu kwa wafanyabiashara hao kuzingatia sheria ya mbolea.

Aidha aliwataka wafanyabiashara hao kuanza maandalizi ya kuuza mbolea za ruzuku inayotarajiwa kutolewa mwezi Julai 2022 na kueleza kuwa wafanyabiashara ndiyo maafisa ugani wa kwanza hivyo wazingatie mafunzo waliyopewa ili waweze kutoa ushauri wa matumizi sahihi ya mbolea kwa wakulima

TFRA MAKAO MAKUU

TFRA kuelimisha wafanyabiashara wa mbolea Jijini Dar es Salaam

Wataalamu kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) kushota Gema Nganyagwa akifuatiwa na Schola Mbalila wakiwa katika ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Temeke kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa wafanyabiashara wa mbolea wa jijini Dar es Salaam.

Mamaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) kupitia sehemu ya Usajili na Leseni imetoa mafunzo kwa wafanyabiashara 255 wa mbolea wa Mkoa wa Temeke ili kuwajengea uwezo katika masuala mbalimbali yanayohusu tasnia ya mbolea.

Mafunzo hayo yaliendeshwa kuanzia tarehe 24-25 Mei, 2022 katika ukumbi wa Halmashauri ya Temeke mkoani Dar es Salaam na tarehe 26 na 27 mafunzo yalifanyika katika ukumbi wa Wizara Kilimo Jijini Dar es Salaam.

Akizungumzia mada zilizowasilishwa kwa wafanyabiashara hao, Meneja wa sehemu ya Usajili na Leseni Scholar Mbalila alisema ni pamoja na majukumu ya TFRA, matumizi sahihi ya mbolea, uhifadhi na utunzaji wa mbolea, afya ya udongo, virutubisho vya udongo, chokaa na matumizi yake pamoja na fursa zilizopo katika tasnia ya mbolea.

Mafunzo haya ni moja kati ya majukumu ya mamlaka yenye lengo la kuwajengea uwezo wadau wa mbolea na kuwawezesha kujihusisha na biashara ya mbolea pasipo kukiuka kanuni na sheria zinazosimamia tasnia hiyo na hivyo kuepusha madhara yanayoweza kutokea kwa walaji kutokana na ukiukwaji huo.

Wafanyabiashara wa mbolea wakifuatilia mada iliyokuwa ikiwasilishwa na wataalamu kutoka TFRA hivi karibuni.

KANDA YA KASKAZINI

Wadau wa mbolea waishukuru TFRA kuwapa elimu ya mbolea

Kaimu Meneja wa Kanda ya Kaskazini, Gothard Sammy Liampawe (mbele hana cheti) akiwa katika picha pamoja na wanufaika wa mafunzo yaliyofanyika wilayani simanjiro leo tarehe 18 Mei, 2022.

Washiriki wa mafunzo ya matumizi sahihi ya mbolea yaliyoandaliwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) Kanda ya Kaskazini wameishukuru kwa mafunzo mbalimbali yanayotolewa kwa wadau wa mbolea kuhusu tasnia hiyo.

Wametoa shukrani hizo jana tarehe 16 Mei, 2022 walipohitimisha mafunzo na kutunukiwa vyeti vya ushiriki wa mafunzo yaliyofanyika katika ukumbi wa Babati Mjini Mkoani Manyara.

Akielezea mwitikio wa wadau kwenye mafunzo hayo, Kaimu Meneja wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania Kanda ya Kaskazini Gothard Liampawe alisema, wafanyabiashara 126 kutoka Mbulu Dc, Mbulu Tc, Hanang' Tc, Babati Dc, Babati Tc walipatiwa mafunzo na kutunukiwa vyeti papo hapo.

Akizungumzia ushiriki wa wafanyabiashara hao, Liampawe alieleza kuwa washiriki wawili miongoni mwao walitoka mkoani Singida ili kujipatia elimu ya mbolea baada ya kuona tangazo la uwepo wa mafunzo hayo.

Aidha, Liampawe alibainisha kuwa miongoni mwa wafanyabiashara walioshiriki mafunzo hayo, wafanyabiashara 20 walisaidiwa kujisajili katika mfumo wa kielekitroniki wa mbolea(FIS) ili kuweza kujihusisha na biashara ya mbolea kwa mujibu wa sheria.

Akizungumza kwa niaba ya wafanyabiashara hao wa Mbolea Manyara Zacharia J. Malley alisema, mafunzo hayo yamekata kiu yao ya muda mrefu ya kutaka kuelimishwa juu ya matumizi sahihi ya Mbolea ili kufanya biashara kwa kukidhi matakwa ya sheria ya Mbolea No 9 ya Mwaka 2009.

Afisa Udhibiti Ubora, Albert Mwaulambo akisisitiza jambo alipokuwa akitoa mada kwa wafanyabiashara 35 wa mbolea walioshiriki mafunzo ya matimizi sahihi ya mbolea yaliyofanyika katika ukumbi wa Halmashauri ua Wilaya ya Simanjiro leo tarehe 18 Mei, 2022 ili kuwajengea uwezo juu ya Sheria, kanuni na taratibu zinazosimamia tasnia ya mbolea nchini.

KANDA YA KASKAZINI

Wadau wa mbolea waishukuru TFRA kuwapa elimu ya mbolea

KANDA YA KASKAZINI

Wasimamizi wa uingizwaji na usafirishaji wa mbolea mipakani watakiwa kusimamia sheria na taratibu

Kaimu Meneja wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) Kanda ya Kaskazini Gothard Liampawe aliwataka wasimamizi wa mbolea zinazoinginzwa nchini na kusafirishwa nje ya nchi kusimamia sheria na taratibu za uingizaji wa mbolea na usafirishaji wa mbolea hizo.

Liampawe alitoa wito huo jana tarehe 24 Mei, 2022 alipotembelea mpaka wa Horohoro (Horohoro One stop centre Tanga) katika Ofisi ya Plant Heathy Service (PHS) zilizopo katika mpaka wa Tanga na kupokelewa Afisa Ubora Mazao Kiyondo Karata.

Aidha, Liampawe aliahidi kuzifanyia kazi changamoto zilizowasilishwa ikiwa ni pamoja na kuwajengea uwezo wa kufahamu namna mfumo wa mbolea wa kielectroniki unavyofanya kazi na kuwapa taarifa ya mabadiliko mbalimbali yanayotokea kwenye usimamizi wa tasnia ya mbolea nchini mara kwa mara.

Akizungumza katika kikao hicho, mwenyeji wao Kiyondo Karata alieleza kufuarahishwa na ujio wa uongozi wa TFRA na kutumia fursa hiyo kuwasilisha changamoto wanazokabiliana nazo katika suala la udhibiti wa mbolea zinazoingizwa na kusafirishwa nje ya nchi.

Alisema changamoto kubwa ni kukosa uelewa wa namna mfumo wa mbolea wa kielektroniki unavyofanya kazi pamoja na kutokuwa na taarifa ya mabadiliko mbalimbali yanayotokea katika suala zima la kusimamia tasnia ya mbolea.

Ziara hiyo ni moja ya majukumu ya wasimamizi na wadhibiti wa mbolea nchini katika kuhakikisha mbolea zinazoingizwa na kusafirishwa nje ya nchi zinakidhi viwango vya kitaifa na kimataifa.

Kaimu Meneja wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Kanda ya Kaskazini Gothard Liampawe (wa kwanza kulia) akiwa katika picha na wataalamu alioambatana nao katika shughuli za uelimishaji walipotembelea mpaka wa Tanzania na Kenya wa Horohoro mkoani Tanga. Wa pili kushoto ni Afisa Ubora Mazao Kiyondo Karata tarehe 24 Mei, 2022.

NYANDA ZA JUU KUSINI

Wafanyabiashara 120 Nyanda za Juu Kusini wapatiwa mafunzo

Mdhibiti Ubora akitoa mafunzo ya namna ya kusajili mbolea mpya na visaidizi vyake pamoja na kujisajili kufanya biashara ya mbolea TFRA Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ilivyoendesha mafunzo hayo tarehe 30 na 31 Mei, 2022 katika Halmashauri ya Makambako Mkoani Njombe.

Imeelezwa kuwa Mei 30 na 31 uongozi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini wameendesha mafunzo kwa wafanyabiashara 120 wa mbolea wanaopatikana katika ukanda huo.

Hayo yameelezwa leo tarehe 31 Mei, 2022 na Kaimu Meneja wa TFRA wa Kanda hiyo, Michael Sanga mara baada ya kukamilisha siku ya kwanza ya mafunzo yanayoendelea mjini Makambako Mji Mkoani Njombe.

Mafunzo hayo ya siku mbili yanayoendelea yanafanyika katika ukumbi wa Halmashauri ya Makambako yenye lengo la kuwajengea uwezo wafanyabiashara wa mbolea ili Kukidhi matakwa ya kisheria katika biashara ya pembejeo, kutambua makundi ya virutubisho vya mmea na umuhimu wake, kutambua na kuelewa makundi mbalimbali ya Mbolea.

Malengo mengine ya mafunzo hayo ni kutambua taratibu na kanuni za kufuata na kuzingatia wakati wa uanzishaji na uendeshaji wa biashara ya Mbolea.

Akizungumzia matarajio ya mafunzo hayo Afisa Udhibiti Ubora Henerico Renatus anasema ni pamoja na kuongezeka kwa watoa huduma wenye uelewa juu ya matumizi sahihi ya mbolea, kuimarika kwa usimamizi wa ubora wa mbolea, kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao, kuongezeka kwa ushindani katika biashara ya Mbolea na kuongezeka kwa upatikanaji wa mbolea Bora kwa mkulima kwa wakati.

Wafanyabiashara wa mbolea wakifuatilia mafunzo yaliyofanyika katika Ukumbi wa Halmashauri ya Makambako mkoani njombe hivi karibuni.

NYANDA ZA JUU KUSINI

TFRA yakiri upatikanaji mzuri wa mbolea Nyanda za Juu Kusini

Kaimu Meneja wa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini-Mbeya Michael Sanga akiambatana na watumishi wa ofisi yake leo tarehe 16 Mei, 2022 wametembelea maghala ya kampuni ya mbolea ya ETG na kubaini uwepo wa mbolea ya kutosha katika maghala hayo.

Uongozi huo umefanya ziara hiyo ikiwa ni ukaguzi wa kawaida wenye lengo la kujionea endapo biashara ya mbolea inafanyika kwa kufuata sheria na taratibu zinazosimamia tasnia hiyo.

Akitoa takwimu za mbolea iliyopo katika maghala ya ETG Sanga alisema kuna mbolea aina ya DAP tani 208.78, UREA tani 99.68, N: P: K tani 313.10, TSP tani 58.25, SA tani 25.55, MOP tani 20.8 na KYNOPLUS tani 0.85.

Ziara hii ni sehemu ya utekelezaji wa majukumu ya kuhakikisha wakulima wanapata mbolea bora na inayokidhi mahitaji yao kwa wakati.

Shehena za mbolea zikiwa katika maghala mkoani Mbeya